# UrithiWETU

11 MAKOSA YANAYOTOKANA NA KUTOZINGATIA ALAMA ZA UAKIFISHAJI
14 NDUNA SONGEA MBANO, SHUJAA WA WANGONI

# Ufugaji kisasa utaongeza maziwa, nyama, utapunguza hewa ukaa



Watafiti na wadau wa mifugo wakiwa katika picha ya pamoja na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) katika mkutano wa kuboresha mbari na malisho ya mifugo.

**Na Hamisi Kibari**

UPUNGUFU uliopo katika ufugaji wa asili ni pamoja na uzalishaji wa mazao ya mifugo; maziwa, nyama, kwato na ngozi, kuwa madogo na duni.

Ufugaji wa kienyeji pia umekuwa chanzo cha migogoro baina ya wakulima na wafugaji kutokana na wafugaji kuhitaji eneo kubwa la malisho na wakati mwingine, hususani wakati wa kiangazi, wafugaji kuingia kwenye mashamba ya wakulima au maeneo mengine yasiyoruhusiwa kama hifadhi za taifa.

Kwa mujibu tafiti, ufugaji huu wa kienyeji, pamoja na kusababisha changamoto zote zilizotajwa hapo juu, unachangia sana uzalishaji wa hewa ukaa na kusababisha ongezeko la joto duniani ambalo ni chanzo cha mabadiliko ya tabianchi.

Inaendelea Uk. 13

Scanned with CamScanner

